

KUFANYA MABADILIKO

Miradi ya takataka Zanzibar

Sura hii itakupa utangulizi wakufanya vizuri kwa miradi ya takataka ambayo inaendeshwa Zanzibar – kuwa na hamu na ushiriki!

1. Jumuiya ya Mabaki na Mazingira Zanzibar (ZASEA)



Hii ni jumuia isiyo ya kiserikali ni (ZASEA) na ni kiwanda cha mwanzo kidogo kilichoundwa 2010 Zanzibar kusarifu plastiki. ZASEA inalenga ukusanyaji na usafirshaji wa mabaki ya plastiki, kutoa elimu na hifadhi ya mazingira na iliundwa kutokana na uongezekaji mkubwa wa takataka za plastiki hapa Zanzibar. Kiwanda pia kinatoa fursa za ajira kwa wanajamii.



(© Ulli Kloiber)

Hivi ndivyo inavyofanya kazi:

ZASEA ITAKULIPA WEWE kwa chupa kongwe za plastiki, chuma cha pua na keni za aluminiamu, mabaki ya vyuma, vifaa mbali mbali vya magari na betri! Angalia bei kwenye kiambatisho.


Lete vitu vyako vya kusarifiwa tena kwenye kituo chetu cha kusarifi tena ZASEA recycling centre, kilichopo Mombasa kwa mchima maeneo ya kiwanda.

ZASEA iko wazi siku za Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 3.00 asubuhi mpaka 11.00 jioni. Hata hivyo tafadhalii piga simu Na.0773814736 au 0777879723 kwa kuhakikisha.

Wafanyakazi wa ZASEAwatakupimia mzigzo wako chakavu na kuku-lipa fedha taslim kwa chupa zako za plasstiki na mabaki ya vyuma.

Tafadhalii kosha mabaki ya chakula katika vikopo ili kuhifadhi taka zisivawute wadudu.

ZASEA hivi sasa hainunui takataka zilizoshikamana na plastiki, mifuko ya plastiki na vigae hadi hapo tutapowataarifu kwa siku za usoni.



2. ZANREC

ZANREC ni mshughulikaji wa takataka na inafanyakazi Zanzibar na inalenga katika ukusanyaji wa takataka, kuyeyusha na kuuza takataka zinazoweza kusarifiwa kitaifa na kimataifa. ZANREC imejikubalisha kusafisha mazingira ya mji wa Zanzibar kwa kufanya mambo yafuatayo:

- Kwa kutoa huduma nzuri ya hali ya juu katika ukusanyaji wa takataka katika sehemu za biashara na mahoteli. Huduma hii inagharimiwa na wafanya biashara ambao ni mbadala wa kutupa taka katika mazingira.
- Kwa kufanya kazi na jamii kuhakikisha kuwa takataka wanazozikusanya zinashuhulikiwa kwa dhamana. Kikundi cha jamii (jamii, skuli, au klabu ya mpira) kuwasiliana na ZANREC ili wajue kuwa kuna vitu vinataka kukusanya. ZANREC watakwenda na kuvikusanya. ZANREC watakilipa kikundi kutokana na wingi na thamani ya bei kwa wakati husika.
- Kwa kufanya kazi na serikali, jumuia za kimataifa zisizokuwa za kiserikali kuhakikisha kuwa sheria halisi inayo tafsiri takataka imetungwa na elimu ya mazingira inafundishwa maskulini.



(© Zanrec)

KUFANYA MABADILIKO

3. Afrika ya mashariki endelevu (SEA)



Afrika ya mashariki endelevu ni mpango wa ushirikiano uliopo Zanzibar unaosaidia jumuia za kijamii zisizokuwa za kiserikali, skuli na jamii kwa kujenga maisha endelevu ya baadae. Waanzilishi wengi wamelenga kuen-deleza udhibiti wa takataka na kuwasidia washirika kwenye jamii zao kuweka usafi na kunufaika kutokana na usafishaji (recycling), kama vile;

Mansipaa Jamii Vikokotoni ni jumuiya ya mji Mkongwe wa Zanzibar inayofanya kazi ya kusafisha vichochoro katika shehia zao. Wajumbe (wanachama) 30 kila siku wanafanyakazi ya kufagia na kukusanya takataka na vifaa vinavyosarifika vilivyo-tengwa na kuviuza au kutmika tena kama vitu vipyta. Shughuli hizo zinafadhiliwa kupitia huduma za usafishaji mitaro, utengenezaji wa mapambo kutokana na takataka za karatasi, na **makaa kutokana na unga wa makaa**.



(© Nell Hamilton)

Katika kijiji cha **Mwera** SEA imetengeneza matangi 2 makubwa yenye ujazo wa litu 10,000 kwa chupa tupu za plastiki zilizojazwa udongo badala ya kujenga kwa matofali. Kwa Tanzania ni wa kwanza!

SEA vile vile inafanya kazi na taasisi ya utoaji misaada na ujifunzaji wa matarajio (**Prospective Learning and Charitable Institution - PLCI**) kuanzisha na kuendesha klabu za mazingira za skuli. Klabu inafanya ziara za kimasomo kujifunza mambo ya kimazingira, kufanya shughuli za usafishaji katika jamii zao, na wamejenga bustani ya mimea midogo midogo na mbogamboga kwa ajili ya chakula na mfuko wa skuli. PLCI vile vile wamebuni na kutengeneza vitu vya mapambo (jewellery) na ufundi kwa kutumia takataka kama vikopo vya soda, vya aluminiamu na karatasi, ambavyo hatimae huuzwa kwa watalii kwenye vituo vya utamaduni na sanaa hapa Zanzibar.

KITUO CHA SANAAN ZANZIBAR - Cultura Arts Centre Zanzibar (CACZ) ni karakana inayoendeshwa bila faida, sehemu ya kufanya sanaa na duka iliopo mji mkomgwe ambayo inaendesha warsha na mafunzo juu ya utengenezaji sanaa na kazi za ufun-di kwa kutumia vifaa vinavyosarika kama vile, herini kutokana na vikopo vya soda, vidani kutoka magazeti yaliyokwishatumiwa na karatasi zinazosarifika kufanyiwa magamba ya vitabu, ambayo baadae huuzwa kwa watalii.



4. Kituo bunifu cha ufumbuzi wa matatizo (CSRC)

Kituo hiki cha ufumbuzi wa matatizo (ya kimazingira) ni kituo kisicho cha kiserikali cha kujifunzia kilichoko Mangapwani. Ni jumuia ya watu wakawaida katika jamii ambapo wanachama wa sanaa na elimu hupewa mafunzo ya kuwasaidia wao kujihimili wenywewe.

CSRC imejifunga na falsafa ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo kwa kujisaidia wenyewe. Pamoja na madarasa ya compuyuta, lugha na ushonaji, kituo cha CSRC kinafundisha kazi za ujuzi na kutengeneza vitu vya kazi za sanaa vya ajabu kutokana na takataka kwa kutumia plastiki, vigae (glass) karatasi na vitu vyengine. Wasiliana nao uweze kujua mafunzo yanayotolewa hivi sasa na uchaguzi wa mafunzo.



(© Aida Ayers)

5. CHUO CHA ELIMU YA AFYA / KILABU YA MAZINGIRA

Chuo cha elimu ya afya cha Zanzibar kina klabu ya mazingira iliyochangamka vizuri ambayo ni kiongozi kwa kuendeleza shughuli za kusarifu na kurejea matumizi ya plastiki na karatasi kwa kufanya vipimo vitatu vya ufundishaji. Timu ya elimu ya uhifadhi wa mazingira wa kisiwa cha Chumbe iliwapatia mafunzo, wanafunzi wa-meanza kufanyakazi ya kufundisha vilabu vyengine vya mazingira kama elimu rika namna ya kutengeneza zana za kufundishia kwa kutumia vitu vinavyosarifika.



(© Ulli Koiber)